

Lahaja hii hujulikana pia kwa jina la Kikae. Katika baadhi ya maandiko ya zamani jina lililotumika sana ni Kihadimu. Hata hivyo jina la Kihadimu kwa sasa halitumiki sana kwa kuwa linanasibishwa na utumwa.

NADHARIA YA Mwingilianotanzu katika uhakiki wa fasihi simulizi

F. C. N. S. Wanjala
Chuo Kikuu Cha Egerton
simiyu57@yahoo.com

Ikisiri

Nadharia ya Mwingilianotanzu inashikilia kuwa, kazi yoyote ya fasihi simulizi hujengwa kwa kuvunja mipaka ya kitanzu ili kuibuka na kazi mahuluti. Hii ina maana kuwa, hakuna kazi ya fasihi simulizi ambayo inaweza kukamilika bila kuchanganyikana na kazi nyinginezo za fasihi. Malengo makuu ya nadharia hii ni kupinga uchambuzi wa utanzu mmoja mmoja wa fasihi simulizi kana kwamba upo utanzu unaoweza kujisimamia kiutendakazi bila kuingiliana na tanzu zingine. Kwa kawaida, mkabala wa kutenganisha tanzu za fasihi simulizi ndio ambao umezoeleka katika tafiti na chambuzi nyingi za kazi za fasihi simulizi. Nadharia hii inapendekeza kuwa, uainishaji wa Ki-Aristotle wa kutenganisha tanzu, unafaa kuishia katika kiwango cha kidhahania tu, ambacho kitawawezesha watafiti na wachambuzi wa fasihi simulizi, kutambua namna ‘tanzu’ hizi dhahania zinavyoingiliana katika kazi maalum ya fasihi simulizi. Kimsingi, fasihi simulizi ni mfumo timilifu wa maarifa unaotekeleza wajibu wake kupitia mifanyiko mbalimbali ya kitanzu; ambayo ndiyo nguzo kuu ya nadharia hii. Kwa hivyo, ni vigumu kuweka mipaka bayana baina ya tanzu za fasihi simulizi kwa kuwa kila utanzu huibuliwa, hukuzwa na kufifia ndani ya utanzu mwingine unaofanya vivyohivyo ndani ya utanzu mwingine, katika mifanyiko hii ya mahusiano ya kingazi isiyokuwa na mwisho. Vilevile, ujitoshelezaji wa utanzu wowote ule wa fasihi simulizi umo ndani ya uwezo wake wa kusheheni tanzu nyingi katika hali halisi. Kwa hivyo, utenda kazi wa kazi yoyote ya fasihi simulizi unategemea uwezo wake wa kuvunja mipaka dhahania kati ya tanzu ndani mwake.

Maneno muhimu: *nadharia, mwingilianotanzu, mifanyiko ya kitanzu*